ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA

## UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA TAMKO LA KUSAMEHE RIBA NA ADHABU, 2025.

**Zanzibar, 30 Julai , 2025.**

### 1.0 UTANGULIZI:

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inapenda kuwataarifu Walipakodi pamoja na Umma kwamba, Serikali kupitia Tamko Nam. 84 la Mwaka 2025, imeamua **kufuta Riba na Adhabu** kwa Walipakodi wote wenye malimbikizo ya Madeni ya Kodi katika Mamlaka ya Mapato Zanzibar.

### 2.0 MUDA NA UTEKELEZAJI:

Msamaha wa Riba na Adhabu utakuwa kwa muda wa miezi sita kuanzia tarehe **1 Julai, 2025** hadi tarehe **31 Disemba, 2025**. Msamaha wa Riba na Adhabu utahusika na kuwawajibikia walipakodi ambao wametimiza masharti na taratibu ambazo zitajadiliwa na kukubalika baina ya Kamishna Mkuu na Mlipakodi.

### 3.0 KIWANGO KINACHOHITAJIKA KULIPWA:

Msamaha wa Riba na Adhabu utatolewa kwa **asilimia mia moja (100%)** ya Riba na Adhabu kwa Mlipakodi, ambapo Mlipakodi huyo atahitajika kulipa kiwango cha kodi ikiwa ni deni halisi baada ya kutolewa kwa Riba na Adhabu.

### 4.0 UTOAJI WA HUDUMA

Kama ilivyokawaida, Ofisi za ZRA zinakuwa wazi siku zote za kazi; **Jumatatu hadi Ijumaa** kuanzia **saa mbili asubuhi (2:00)** hadi **saa kumi na moja jioni (11:00)** ambapo watahudumiwa na Kamati maalum iliyoteuliwa kufanyakazi hii. Fomu za kuomba punguzo hilo zitakuwa zikitolewa na kurejeshwa katika ofisi zetu kama zilivyoainishwa hapa chini;

- **4(a). Kwa Walipakodi wanaopata huduma kupitia Ofisi za ZRA Unguja, wanatakiwa wafike katika Jengo la ZRA Mazizini Chumba Nam.104 na 105.**
- **4(b). Kwa Walipakodi waliopo Pemba, wanatakiwa wafike katika ofisi za ZRA Gombani Pemba chumba Nam. 13.**

### 5.0 HITIMISHO:

ZRA inawaomba na kuwahimiza walipakodi wote wenye malimbikizo ya madeni ya kodi kutumia fursa hii iliyotolewa na Serikali kulipa madeni hayo ndani ya muda uliotolewa. Hii itawasaidia kuanza upya na kupanga mienendo ya biashara zao bila bughudha na kuwapa utulivu.

**"Tulipe Kodi kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

IMETOLEWA NA

**KITENGO CHA HABARI, UHUSIANO NA HUDUMA KWA MLIPAKODI**
**MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR**